
# MASWALI YANAYOULIZWA SANA KUHUSU COVID-19

HEARTLAND HEALTH CENTERS
HEALTHCARE FROM THE HEART

## 1 Je, chanjo itanipa COVID-19?

Hapana. Chanjo haina virusi hai. Huwezi kuambukizwa wala kuwaambukiza wengine virusi vya COVID-19 ukipokea chanjo ya COVID-19. Chanjo huusaidia mwili wako kuzalisha protini inayoufunza mwili wako kupambana na virusi.



## 2 Je, ninahitaji kupata chanjo ikiwa tayari nimekuwa na COVID-19?

**Ndiyo.** Hata ikiwa umekuwa na COVID-19, kuna uwezekano wa kuipata tena. Wanasayansi hawajui ikiwa utakingwa milele wapo tayari umekuwa na COVID-19. Kupata chanjo kutapunguza uwezekano wa kupata COVID-19 tena.

## 3 Kilicho katika chanjo

Chanjo za Moderna na Pfizer zina kitu kinachoitwa mRNA, kinachousaidia mwili wako kujifunza jinsi ya kukabiliana na virusi vya COVID-19. mRNA SI virusi na haitabadilisha DNA yako. Chanjo ya Johnson & Johnson hutumia virusi tofauti visivyo na madhara kuusaidia mwili wako kujifunza jinsi ya kukabiliana na COVID-19. Hakuna kisilikoni wala kitu kingine katika chanjo kitakachokufuatilia.

## 4 Nikipata chanjo, je, hii inamaanisha sitawahi kupata COVID-19?

**Hapana.** Chanjo tulizo nazo sasa ni bora sana, lakini bado kuna uwezekano mdogo kuwa unaweza kupata COVID-19 baada ya kupata chanjo. Hii ni sawa na chanjo nyingine, kama chanjo ya mafua. Hata kama umepokea chanjo, bado ni muhimu kuendelea kuvaa barakoa, kudumisha umbali na watu wengine na kunawa mikono vizuri ili kujikinga mwenyewe dhidi ya kuwa mgonjwa.




## 5 Je, chanjo ya COVID-19 hufanya nini?

Chanjo ya COVID-19 haina virusi, lakini ina protini zinazousaidia mwili wako kujifunza jinsi ya kupambana na virusi vya COVID-19. Wakati mwili wako unapojifunza jinsi ya kupambana na virusi, unajenga kingamaradhi. Kwa njia hiyo, ukiwa kwenye hatari ya maambukizi ya virusi, mwili wako utajua jinsi ya kupambana nayo ili usiwe mgonjwa.

## 6 Je, tunaweza kuiamini chanjo hata ingawa ilitengenezwa haraka?

**Ndiyo.** Muda, pesa na utafiti mwingi wa kisayansi kuhusu aina hii mpya ya chanjo vilitumika kutengeneza chanjo hii. Chanjo hii ilijaribiwa kwa maelefu ya watu jasiri waliojitolea ili kuhakikisha kuwa ilifanya kazi kabla ya kuupa umma. Hili ni jambo la kawaida. Chanjo nyingine zote, kama vile chanjo ya mafua, pia zinatengenezwa haraka na bado zinafanya kazi.



## 7 Je, kuna madhara ya chanjo?

Watu wengine wanaweza kuwa na madhara ya chanjo, jambo ambalo ni la kawaida kwa chanjo yoyote. Madhara ya chanjo kwa kawaida ni ishara kwamba mwili wako unaunda kingamaradhi. Madhara ya chanjo yanaweza kujumuisha maumivu, wekundu na kuvimba sehemu ya sindano, uchovu, maumivu ya misuli, maumivu ya viungo, homa, kichefuchefu, unyonge na vinundu vya limfu. Madhara ya chanjo yanaweza kuwa makubwa baada ya chanjo ya pili, ikiwa umepata chanjo ya dozi mbili. Madhara ya chanjo ya muda mrefu hayajulikani, lakini chanjo nyingi hazina madhara ya muda mrefu.

## 8 Je, unaweza kupata chanjo ukiwa na mizio?

**Ndiyo, lakini...**Zungumza na daktari wako kabla ya kupata chanjo ikiwa una wasiwasi kuhusu au una historia ya mikabiliano ya mizio. Ingawa mikabiliano mibaya ya mizio haikuonekana katika majaribio ya matibabu ya chanjo ya COVID-19, mikabiliano adimu ya mizio kwa chanjo kwa jumla inawezekana. Chanjo ya COVID-19 haina bidhaa yoyote ya mnyama kama vile mayai.

## 9 Je, mfumo Wangu binafsi wa kingamaradhi unaweza kunikinga?

**Hapana.** COVID-19 imesababisha ugonjwa mbaya sana na vifo kwa watu wengi. Uko kwenye hatari kubwa ya COVID-19 usipopata chanjo. Ukipata COVID-19, pia uko kwenye hatari ya kuwaambukiza wapendwa wanaoweza kuugua sana. Kupata chanjo ya COVID-19 ni chaguo salama sana.

## 10 Je, watoto wanaweza kupata chanjo?

**Ndiyo!** Vijana wa miaka 12 na zaidi wanaweza kupata chanjo ya Pfizer. Chanjo ya watoto wachanga chini ya miaka 12 bado haijapatikana

## 11 Je, kuna chanjo ambayo ni bora kuliko nyingine?

**Hapana.** Chanjo zote tatu zinafanana sana na zinafanya kazi sawa. Inapendekezwa kupata chanjo yoyote unayopewa. Ukipata Pfizer au Moderna, hakikisha kuwa umepata dozi zote mbili za chanjo ya aina moja.

## 12 Je, chanjo hii inaweza kunikinga dhidi ya kupata aina mpya za virusi?

Inawezekana Zaidi. Wanasayansi wanaamini kuwa chanjo zote tatu zitakukinga dhidi ya kupata aina mpya za COVID-19.

## 13 Je, ni dozi ngapi zinazohitajika na kwa nini?

Chanjo za Pfizer na Moderna zinahitaji sindano mbili za chanjo sawa. Sindano ya kwanza inakupa kinga na kuusaidia mwili wako kutambua virusi, lakini bado uko kwenye hatari ya kupata COVID-19 mbaya hadi upate sindano ya pili. Chanjo ya Johnson & Johnson inahitaji tu dozi moja.

## 14 Je, ninaweza kupata chanjo nikiwa mjamzito au nikinyonyesha?

**Ndiyo, lakini...** Zungumza na mtoa huduma wako wa matibabu kabla ya kupata chanjo ikiwa wewe ni mjamzito au unanyonyesha. Atakusaidia kufanya uamuzi unaofaa kwa ajili yako na mtoto wako.

## 15 Je, chanjo ni ya malipo?

**Hapana.** Chanjo ni ya BILA MALIPO kwa kila mtu, hata ikiwa huna bima na bila kujali hali yako ya uhamiaji.

## 16 Je, nitahitajika kupata chanjo?

**Hapana.** Chanjo haihitajiki. Hata hivyo, kadri watu zaidi wanavyopata chanjo, ndivyo hatari zinavyokuwa za chini kwa yeyote kupata COVID-19.

# JE, UNAWEZA KUFANYA NINI?

Ikiwa ungependa kufahamu mengi kuhusu Chanjo ya COVID-19, mahali unapoweza kupata chanjo na taarifa kuhusu COVID-19, tembelea www.heartlandhealthcenters.org/coronavirus au piga simu (773) 751-7800